

ZINGATIENI WELEDI ILI MUISAIDIE SERIKALI-KAMATI YA BUNGE

Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Katiba na Sheria imeutaka Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini nchini – RITA kuhakikisha inazingatia weledi katika kutekeleza majukumu yake.

Rai hiyo imetolewa mjini Dodoma na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Joseph Mhagama baada ya RITA ikiongozwa na Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba Kabudi kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mhagama amesema RITA wakifanya kazi yao kwa kuzingatia weledi na umakini mkubwa wataiwezesha Serikali kuondokana na usajili mpya wa kupata vitambulisho vya taifa kama ilivyo sasa kwani wananchi wote watakuwa wamesajiliwa na kuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Awali akiwasilisha taarifa yake Kaimu Mtendaji Mkuu wa RITA Bibi Emmy Hudson alisema Wakala wake umejipanga kuhakikisha usajili wa Watanzania wote wanasajiliwa na kuwa na vyeti vya kuzaliwa ambapo usajili wa watoto chini ya umri wa miaka mitano umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 10 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 81 mwaka 2017.

Amesema RITA kwa sasa inaboresha Mfumo wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu ambao unalenga kusogeza huduma za usajili wa matukio muhimu ya binadamu karibu na wananchi , kuboresha ukusanyaji wa takwimu na matumizi ya TEHAMA katika huduma hizo.

Amesema kwa sasa RITA inatekeleza Mpango wa usajili wa watoto chini ya miaka mitano; kusajili vizazi na vifo kupitia TEHAMA na kusajili watoto waliopo shuleni wenye umri kuanzia miaka 5-18.